
# Matendo ya Mitume 1




Published by the Comic Bible Society, LLC
Copyright © 2021

Kingstone Comics maintains copyright to this comic book as provided by United States copyright law.

Print and digital copies of this version may be freely distributed without penalty under a Creative Commons license.


THEOFILO MKUU, KILE KITABU CHANGU CHA KWANZA NILIANDIKA MAMBO YOTE ALIYOYAFANYA NA KUYAFUNZA YESU MPAKA SIKU ALIYOCHUKULIWA JUU MBINGUNI.
"KUPITIA ROHO MTAKATIFU, YESU ALIWAPA MAAGIZO WALE MITUME ALIOWACHAGUA."
"ALIVYOFUFUKA KUTOKA MAUTINI ALIJIDHIHIRISHA KWA WATU HAWA NA KUWAPA USHAHIDI MWINGI WA KUWAHAKIKISHIA KAMA KWELI ALIKUWA HAI."
"WAKTI HUU ALIONEKANA NA ZAIDI YA 500."
"PIA ALIWAPA AMRI YA WAZI..."
...MSIONDOKE MJI WA YERUSALEMU ILA NGOJENI ZAWADI BABA YANGU ALIAHIDI NA NILIYOWAAMBIA KUIHUSU.
YOHANA ALIWABATIZA NA MAJI LAKINI SIKU CHACHE ZIJAZO MTABATIZWA NA ROHO MTAKATIFU.






MATENDO 1:6-10




MATENDO 1:12-19


KITABU CHA ZABURI CHASEMA K UWA MAHALI PAKE PANAFAA KUACHWA...
...NA KUWA MWENGINE ANAFAA KUCHUKUA MAHALA PAKE.
TUNAFAA KUMCHAGUA MTU AMBAYE AMEKUWA HAPA TANGU MWANZONI-----
NAMPENDEKEZA YOSEFU - ALIONA KUFUFUKA KWA MACHO YAKE.
NDIO, NA MTU MZURI.
NAMI NAMPENDEKEZA MATIYA. AMEJAWA NA IMANI NA ROHO MTAKATIFU.




MATENDO 1:24-26


"WAKATI WAYAHUDI WALIPOSHEREHEKEA PENTEKOSTE (MWISHO WA KUVUNA NAFAKA) WAFUASI WALIKUSANYIKA WOTE PAMOJA."
"UPEPO MKALI ULITOKA MBINGUNI UKAIJAZA NYUMBA WALIMOKAA - NA NDIMI ZA MOTO ZILITUA JUU YA KILA MMOJA WAO."
"WAYAHUDI WACHA-MUNGU WALIKUJA PAMOJA WAKIKIMBIA WALIPOSIKIA SAUTI."
NAMSIKIA KWA LUGHA YANGU - KIMEDI - AKITANGAZA UKOMBOZI KATIKA MTU HUYU YESU.
NAMI NASIKIA KIFRIGIA - AKISEMA MUNGU ANAVYOWEZA KUSAMEHEA DHAMBI ZANGU.
NAYASIKIA MAAJABU YA MUNGU KWA NDIMI YANGU YA KIELAMI!


"KILA MMOJA ALIANZA KUONGEA LUGHA ZENGINE ALIVYOWAWEZESHA ROHO MTAKATIFU."
WAMEKUNYWA DIVAI NYINGI!
NDIO - WAMEKUNYWA SANA KWENYE SHEREHE.


"MVUVI PETERO ALISIMAMA KUZUNGUMZA. ALIKUWA AMEBADILIKA."
"MANENO ALIYOYASEMA SIKU HIYO YAIKUWA YA KUFAA...."
WATU HAWA HAWAJALEWA MNAVYOFIKIRIA - NI SAA TATU ASUBUHI TU!
HIKI NI KILICHOZUNGUMZWA NA NABII YOELI - KUWA MUNGU ATAMWAGA ROHO WAKE SIKU ZA KIAMA.


KUTAKUWA NA MAAJABU KWENYE MBINGU JUU NA ISHARA ULIMWENGUNI CHINI.
NA KILA ANAYELIITA JINA LAKE ATAKOMBOLEWA.
ACHENI ISRAELI YOTE IJUE - MUNGU AMEMFANYA HUYU YESU MLIYESULUBISHA, BWANA NA KRISTO.
TUBU NA MBATIZWE - KILA MMOJA WENU - KATIKA JINA LA YESU KRISTO KWA MSAMAHA WA DHAMBI.
KISHA MTAPOKEA ZAWADI YA ROHO MTAKATIFU.






MATENDO 2:42-47



LAKINI HUU ULIKUWA MWANZO TU...
"SIKU MOJA PETERO NA YOHANA WALIPOKUWA WANATEMBEA HEKALUNI WALIONANA NA MTU ALIYEKUWA ANAOMBA."
SIWEZI KUFANYA KAZI, TAFADHALI... NAHITAJI PESA ZA KUJILISHA.
SINA DHAHABU WALA FEDHA, LAKINI NILICHONACHO - NITAKUPA.
KATIKA JINA LA YESU KRISTO WA NAZARETI - TEMBEA.


MATENDO 3:1-6






MATENDO 3:1-10




MATENDO 3:11-26



ALIKUWA KILEMA JANA - NILIMUONA!
MIMI PIA - NILIMPA PESA LEO ASUBUHI TU.
NILIMSIKIA YULE MVUVI AKILITUMIA JINA LA YESU ALIPOMPONYA MTU YULE.
HAIWEZEKANI.
"SASA HAYO YAMEPATA UMAKINI WA WAMILIKI AMBAO HAWAKUMJALI YESU, HATA ZAIDI KWA KUWA MITUME WALIENDELEA KUZUNGUMZA KATIKA JINA LAKE."
MFUNGE. HUYO ALIYE NA KIWETE...AAH... ALIYEKUWA KIWETE.
MSHIKE MWENZAKE PIA. WAWEZA KUKESHA JELA.
BARAZA LITAKUTANA KESHO.
LAZIMA KUNA JAMBO NA HUYU MTU YESU.
MBONA WAKUU WALIMSULIBISHA HATA HIVYO?
...LAKINI ALINIPONYA.
WAFUASI WAKE WASEMA BADO YU HAI.
"VIONGOZI WA KIDINI HAWAKUFURAHIA. WAFUASI WA KRISTO WAMEKUWA MPAKA TAKRIBANI 5000."
"BILA HAKIKA WATAFANYAJE, VIONGOZI WALIWAFUNGA PETERO NA YOHANA."




MATENDO 4:1-4




MATENDO 4:5-12




MATENDO 4:13-22


"MANENO YA MAKUHANI HAYAKUTIMIZA WALICHOTARAJIA."
"MITUME WALIANZA KUOMBA NA KUMTAFUTA MUNGU ZAIDI."
MUNGU MKUU, ULIUMBA MBINGU NA NCHI NA BAHARI, NA KILA KITU HUMO NDANI.
MBONA MATAIFA YAKASIRIKA NA WATU WAPANGA BURE?
VIONGOZI WALIUNGANA DHIDI YA MTUMISHI WAKO MTAKATIFU YESU - LAKINI WALIFANYA ULICHOKUWA UMEPANGA HAPO MBELENI.
SASA ONA VITISHO VYAO NA UWARUHUSU WATUMISHI WAKO KULIZUNGUMZIA NENO LAKO KWA USHUPAVU WOTE.
UNYOSHE MKONO WAKO KUPONYA NA KUTENDA ISHARA ZA MIUJIZA NA AJABU KATIKA JINA TAKATIFU LA MTUMISHI WAKO YESU.
"MUNGU ALIKUWA KAZINI."
"CHUMBA KILIKUWA CHATINGISIKA WALIPOMALIZA KUOMBA."
"WANAFUNZI WALIANZA KUONGEA KWA USHUPAVU KUHUSU KUFUFUKA KWA KRISTO."






MATENDO 4:32-37


"LAKINI MUONGO WA KALE, IBILISI, HAKUKATA TAMAA ALIPOENDELEA KUVURUGA KIKUNDI HIKI CHA WAFUASI WA YESU."
TUSEME TULIPATA KIWANGO HIKI TULIPOLIUZA SHAMBA.
UNA UHAKIKA? WAT U WATATUFIKIRIA ZAIDI YA TUNAVYOSTAHILI.
ITAINUA SIFA YETU KATIKA JAMII. HAKUNA ATAKAYEJUA.
ANANIA, UNGEWEZAJE KUMRUHUSU IBILISI AJAZE MOYO WAKO ILI UMDANGANYE ROHO MTAKATIFU?
UMEWEKA NYENGINE HUKU UKIJIDAI UMEMPA MUNGU YOTE.
ILIKUWA YAKO KABLA KUUZWA. NA BAADA YA KUUZWA, HELA ZILIKUWA MIKONONI MWAKO.
HUJALAGHAI WANAADAMU - ILA MUNGU.
"MARA TU ALIPOSIKIA HAYA, ANANIA ALIANGUKA NA KUFA. KIFO BARIDI."
"VIJANA WALIKUJA KUMBEBA NA KUMTOA NJE KWA MAZISHI."

MATENDO 5:1-6






MATENDO 5:7-11




MATENDO 5:12-16






MATENDO 5:17-20




MATENDO 5:21-26






MATENDO 5:27-33




MATENDO 5:33-39






MATENDO 5:40-42




MATENDO 6:1-15


"WENGI WA MAKUHANI WA HEKALUNI WALIAMINI INJILI, AU 'HABARI NJEMA' KUMHUSU YESU!"
"WENGI ZAIDI WALIMFUATA YESU SASA KULIKO WALIOMFUATA WAKATI ALIPOKUWA HAI!"
"KWA HOFU WASHIRIKA WA BARAZA TAWALA, WALIKUSANYIKA KUAMUA WATAKALOLIFANYA."
"KUHANI MKUU ALIWAALIKA KIJANA MWENYE HASIRA AMBAYE, ANGEKUWAM BAADAYA YA YOTE HAY, MTUME."
TUMEFIKA MAHALI PA MGOGORO!
KUWASHIKA NA KUWAPIGA HAWA WANAOJIITA MITUME, PETERO NA YOHANA, HAIKUTEKELEZA LOLOTE.
LICHA YA TAHADHARI ZETU WAMEENDELEA KUHUBIRI UZUSHI!
WALISEMA, "LAZIMA TUMTII MUNGU KULIKO BINAADAMU!"
WAFANYA KAMA AMBAYE TU MAADUI WA MUNGU!
WANAKANA MAMLAKA YETU MBELE YA WATU!
MGOGORO HUU WAZIDI KUWA MBAYA ZAIDI KILA SIKU. NIMETEUA SAULI WA TARSO KAPTENI WA ASKARI WA HEKALUNI NA KUMUALIKA AZUNGUMZE NA BARAZA.
WAKUBWA WANGU WALIOHESHIMIKA, WANA WA IBRAHIMU!
YERUSALEMU IMEJAWA NA WAFUASI WA MASSIAH BANDIA, YESU.
WANAINGIA MASINAGOGI YETU NA NYUMBA ZETU WAKIZITIA ZUMU AKILI ZA WATU WETU.
WAKITIA AKILI ZAO SUMU?



MATENDO 5:29


KWA KUFUNGUA MAANDIKO NA MAFUNZO KUHUSU KAFARA YA UKOMBOZI YA MASSIAH?
LA NIKODEMU!
KWA KUSEMA SEREMALA MGALILAYA ALIYEKUFA NI MTEULE WA MUNGU!
MTU ALIYECHINJWA KWA KIMYA KAMA MNYAMA ASIYE NA NGUVU, KASHINDWA NA WAKANDAMIZAJI WETU WA KIRUMI!
ALISHINDWA?
AMA ALIJIPA KWA KIFO - KAMA ALIVYOTAFSIRI ISAYA -- KWA DHAMBI ZA BINAADAMU?
UMEKUWA MFUASI WA SEREMALA, NIKODEMU?
SAULI, NIKODEMU NI MKUU KWENYE BARAZA. ZUNGUMZA NAYE KWA HESHIMA ANYOISTAHILI!
NAELEWA WASIWASI WA SAULI. WAKATI MMOJA NINGEWAZA HIVYO.
IBILISI APENDELEA MASSIAH BANDIA, SIO?
SAULI WA TARSO, NAHOFIA HUNGEMJUA MASSIAH WA ISRAELI HATA KAMA ANGEIVAA TAJI WA MFALME DAUDI NA KUKUGONGA NA FIMBO YA MUSA!
WANANCHAMA WA BARAZA TAKATIFU!
MTASIMAMA HAPA OVYO WAKATI NIKODEMU ANATETEA KUNDI LA HUYU ANAYEKUFURU?


RABBANI GAMALIELI, MJUKUU ALIYEHESHIMIKA WA MAREHEMU HILLELI MKUU.
NILISOMA KWA NYAYO ZAKO MIAKA MITANO.
ULINIFUNZA TORAH NI NJIA, NA UKWELI, NA UZIMA.
ILA SOTE TULIMSIKIA MGALILAYA AKISEMA, "MIMI NDIMI NJIA, UKWELI NA UZIMA; HAKUNA ANAYEKUJA KWA BABA ILA KUPITIA KWANGU,"
ALIKUFA KATIKA JASHO LAKE NA DAMU. JE, TORAH HAISEMI, "AMELAANIWA ANYENING'INIA TOKA MTINI?"
WATU WETU WENGI, VIONGOZI WETU WENGINE, PIA, WATUACHA KUMFUATA MTU ALIYEKUFA!
JE KAMA HUYU YESU... SIO MFU TENA?
TUNAZUNGUMZIA KWA SAUTI IAMNI YETU KATIKA KUFUFUKA HUKU TUKIWAZA HAKUNA MTU ANAYEWEZA KUFUFUKA KUTOKA MAUTI?
AAH! LAKINI HATA HAKUFA.
BASI YUKO WAPI? MWILI WAKE ULIFANYIKAJE?
WAFUASI WAKE WALIUIBA!
WADHANI WALE WAOGA WALIWAZIDIA ASKARI WA KIRUMI WENYE SILAHA NA KULISOGEZA JIWE LILE?
NYUMBA ZA WAFUASI NA MASHAMBA YAMEVAMIWA NA ASKARI WA HEKALU. HAKUNA AKIYEPATIKANA!
NIMESIKIA HAYA MARA NYINGI TAYARI! SITAKI KUYASIKIA TENA!


SEREMALA KUTOKA NAZARETI ALIKUWA ANAKUFURU!
"ANAYEKUFURU" BALI SISI WATATU HAPA PAMOJA NA WENGINE 500, TULIMUONA NA MACHO MWEZI MMOJA BAADA YA KUMUONA AKIFA!
NAWAONYA, TUSIPOVUNJA MAFUNDISHO HAYA WAFUASI WAKE WANAITA INJILI YA REHEMA, ITAKUWA MWISHO WETU NA TUNAVYOISHI!
TUNAFAA TUWAITE WATU WETU WARUDI KWA SHERIA YA MUSA - TUMAINI LAO LA PEKEE LA UKOMBOZI!
AMA NI MUNGU PEKEE ALIYE TUMAINI LAO LA UKOMBOZI?
MUNGU AMBAYE LABDA ALIMTUMA MWANAYE AWE MWANA KONDOO ALIYETOLEWA KAMA DHABIHU KWA DHAMBI ZA DUNIA?
ACHA KUTEMA...
...KUFURU!!!
SAULI! SEHEMU GANI YA SHERIA YA MUSA INAKUAMBIA KUONYESHA DHARAU KWA WAKUBWA WAKO?



MWALIMU GAMALIELI, SI... SIMAANISHI KUKUKOSEA.
SIO KUNIKOSEA KWAKO KUNAFAA KUKUTIA WASIWASI.
JE, MUNGU, HAKIMU WA WATU WOTE, AFIKIRIA NINI KUHUSU CHUKI ILIYOMO MOYONI MWAKO?
JE, HUKUNIFUNZA KUWA LAZIMA TUITETEE SHERIA YA MUNGU NA KUSHIKILIA UKWELI WOTE JUU YA VYOTE?
NAWEZA KUSOMA KUTOKA MAANDIKO YA MANABII?
ISAYA ASEMA KUMHUSU MASSIAH:
"ALIDUNGWA KWA AJILI YA DHAMBI ZETU, ALIVUNJWA KWA AJILI YA UOVU WETU...KWA AJILI YA VIDONDA VYAKE TUMEPONYWA."
"ALIONGOZWA KAMA MWANA KONDOO HADI KWENYE KICHINJIO ... HAKUFUNUGUA KINYWA CHAKE."
"ALIPIGWA KWA AJILI ZA DHAMBI ZA WATU WANGU."
JE, HUKUSEMA YESU ALINING'INIA MSALABANI KAMA MNYAMA ALIYESHIN JWA?
ALIDUNGWA NA WARUMI?
YAWEZEKANA YEYE NDIYE ISAYA ALISEMA ATAKUFA KWA AJILI YA DHAMBI ZA WATU WA MUNGU?
YEYE NDITE MASSIAH? AU...SIYE?
NASEMA... LAZIMA TUNGOJE TUONE.
WAT WANAODANGANYA KUWA WALIKULA NA MUNGU-MTU ALIYEFUFUKA, HAWATAKWAMILIA UONGO HUO USONI WA MATESO YANAYOWANGOJA.
LAKINI KAMA NI MASSIAH ALIYEAHIDIWA, BASI SISI NI NANI KUPINGA MIPANGO YA MUNGU MKUU?
AMEFUNGWA!




ISAYA 53:5, 7-8

"THE BIBLE EXPLAINED
IN EVERY LANGUAGE."





**SUPERBIBLE.TV**